TANGAZO LA SERIKALI Na. 1043 la tarehe 13/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU ANATWANGAINA KUWA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA ANATWANGAINA YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo la Msitu Anatwangaina kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Anatwangaina ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la msitu lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Anatwangaina.

Madhumuni ya tangazo

3. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Taifa Anatwangaina ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu ya uwanda wa chini wa misitu ya Pwani, uwanda wa nyasi na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa

maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Anatwangaina.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza eneo la Msitu Anatwangaina kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Anatwangaina, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA HANDENI


MSITU WA HIFADHI WA TAIFA ANATWANGAINA

Makadirio ya eneo: Hekta 32.56 au Kilometa za Mraba 0.32

Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Anatwangaina unaopatikana Wilaya ya Handeni katika Mkoa wa Tanga kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 3196 (Skeli 1:5,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:


*Tangazo la Serikali Na. 1043 (Linaendelea)*




SCHEDULE

| BEACON NO. | TRUE BEARING | DISTANCE IN METRES | COORDINATES EASTINGS | NORTHINGS |
|---|---|---|---|---|
| FD-01 | | | 390353 | 9425630 |
| | 356°47' | 374.6 | | |
| FD-02 | | | 390332 | 9426004 |
| | 2°9' | 238.2 | | |
| FD-03 | | | 390341 | 9426242 |
| | 96°35' | 383.5 | | |
| FD-04 | | | 390722 | 9426198 |
| | 108°47' | 614.8 | | |
| FD-05 | | | 391304 | 9426000 |
| | 180°0' | 108.0 | | |
| FD-06 | | | 391304 | 9425892 |
| | 204°3' | 286.9 | | |
| FD-07 | | | 391187 | 9425630 |
| | 299°37' | 176.0 | | |
| FD-08 | | | 391034 | 9425717 |
| | 317°23' | 422.5 | | |
| FD-09 | | | 390748 | 9426028 |
| | 252°38' | 33.5 | | |
| FD-10 | | | 390716 | 9426018 |
| | 229°16' | 47.5 | | |
| FD-11 | | | 390680 | 9425987 |
| | 211°44' | 89.4 | | |
| FD-12 | | | 390633 | 9425911 |
| | 231°37' | 61.2 | | |
| FD-13 | | | 390585 | 9425873 |
| | 222°14' | 117.5 | | |
| FD-14 | | | 390506 | 9425786 |
| | 214°57' | 162.3 | | |
| FD-15 | | | 390413 | 9425653 |
| | 249°1' | 64.3 | | |
| FD-01 | | | 390353 | 9425630 |

LOCATION MAP FROM DAR ES SALAAM SHEET SB-37




SCALE 1:250,000

Legend
- Beacons
- Forest reserve boundary
- Contour
- Seasonal river

GPS Survey
Grid : UTM Zone 37S
Datum : ARC 1960
Unit of Measurement : Metres
Topographic Sheetst : 129/1
Surveyed by National Land Use Planning Commission Team, 2022
Verified by Shani Kiluvia, Firady Kibona, Musa Sanga and Wilbroad Kitambala, August 2023
Map drawn by S. Khalid, October 2023
Ministry of Natural Resources and Tourism, Tanzania Forest Services Agency.

Dodoma
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*